JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

## KIKAO CHA AROBAINI NA SABA

**18 JUNI, 2019**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

______________________

## MKUTANO WA KUMI NA TANO

### KIKAO CHA AROBAINI NA SABA – TAREHE 18 JUNI, 2019

## I. DUA:

## II. MASWALI:

**OFISI YA WAZIRI MKUU:**

**390. MHESHIMIWA ESTHER MICHAEL MMASI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Serikali imeonyesha nia madhubuti kupitia mikakati yake ya kuinua ajira kwa Watanzania:-

Je, ni kwa namna gani Serikali imejipanga kuinua ajira kwa Vijana kupitia makundi maalum kama vile Vijana wa kidato cha nne, darasa la saba na waendesha boda boda.

## OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**391. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):- Halmashauri nyingi zina uwezo mdogo wa kujiendesha kwa kutumia mapato yake ya ndani:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutenga fedha katika bajeti ili kuzisaidia Halmashauri kujenga Hospitali na Vituo vya Afya badala ya kuziachia jukumu hilo Halmashauri pekee.

**392. MHESHIMIWA MARTHA MOSES MLATA (VITI MAALUM)**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itazijenga vizuri barabara za Kibaya – Urughu, Urughu – Mtekente na Mtekente – Ndago zilizopo Wilayani Iramba ili kufungua fursa za kiuchumi kwa Wananchi wa eneo hilo.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**393. MHESHIMIWA MBARAKA KITWANA DAU (MAFIA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni Watalii wangapi walitembelea Kisiwa cha Mafia kwa mwaka 2017/2018.

**WIZARA YA NISHATI:**

**394. MHESHIMIWA JULIUS KALANGA LAIZER (MONDULI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

(a) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa REA kama ilivyoahidi katika Vijiji vya Munjere, Baraka, Mbaasha, Lepurko, Mti Mmoja, Arkatan, Arkaria, Mfereji, Ndonyonaado, Mswakini, Naitolia, Emurua, Lashaine, Orkenswa, Engaaroji, Oldonyolengai na Naalarami;

(b) Je, ni lini Serikali itapeleka umeme katika Shule ya Sekondari Oldonyolengai ambayo

laini imefika tangu mwaka 2015 lakini mpaka sasa umeme haujawaka.

**WIZARA YA MIFUGO NA UVUVI:**

**395. MHESHIMIWA SELEMANI SAID BUNGARA (KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:- Uvuvi haramu unazidi kushamiri siku hadi siku hasa kwenye maeneo ya Songosongo, Somanga, Njianne, Kivinje hadi Pwani ya Bushungi; Aidha, kwenye maeneo hayo kuna bomba la gesi linapita na hivyo kujenga hofu ya uwezekano wa mlipuko pamoja na uharibifu wa mazingira kwenye maeneo tajwa:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti kukabiliana na tishio hilo sugu;

(b) Kwa kuwa wanaofanya hujuma hizo wamejiandaa kwa kuwa na boti maalum katika kuendesha hujuma hizo. Je, Serikali haioni haja ya kuleta boti za doria zenye uwezo wa hali ya juu ili kulinda bahari sanchari na bomba la gesi.

**WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:**

**396. MHESHIMIWA SILAFU JUMBE MAUFI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Mgane anapobaki na Watoto hundi zinazolipwa kama kuna malipo huandikwa kwa jila lake lakini kwa Wajane huwa ni tofauti kwani hupewa masharti ya kulipiwa Mahakamani na awe na muhtasari wa Kikao cha upande wa Mwanaume na ndipo malipo yafanyike kwa mgao maalum:-

(a) Je, ni kwa nini jina la Mjane lisiandikwe kwenye hundi na asimame na Watoto wake kwa kupewa haki hiyo;

(b) Je, Serikali haioni kama inamnyanyasa Mjane;

(c) Kama ni Sheria; Je, Serikali haioni kwamba ni wakati wa kuiangalia upya Sheria hiyo.

**397. MHESHIMIWA SAED AHMED KUBENEA (UBUNGO):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:- Serikali ilitangaza kuwa Wanasheria wote waliopo kwenye Mashirika ya Umma watafanya kazi chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kupunguza gharama za uendeshaji wa kesi na kuwapa ufanisi kwenye ufuatiliaji wa kesi zinazofunguliwa dhidi ya Serikali:-

(a) Je, utekelezaji wa agizo la Serikali kuhusu Mawakili binafsi kutosimamia kesi za Serikali umefikia wapi;

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kilichookolewa tangu Mashirika ya Serikali yaache kutumia Mawakili wa nje.

**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:**

**398. MHESHIMIWA IGNAS ALOYCE MALOCHA (KWELA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano:- Barabara ya Ntendo – Muze ni barabara muhimu inayounganisha Mji wa Sumbawanga na Ukanda wote wa Bonde la Ziwa Rukwa; lakini barabara hii inakabiliwa na changamoto nyingi ikiwemo utelezi kipindi cha mvua, miinuko mikali na ufinyu wa barabara katika maeneo ya milimani:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza kilomita zaidi ya mbili za kiwango cha lami;

(b) Je, ni lini Serikali itatoa fedha ili kupanua barabara hii hasa eneo la Mlimani.

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA:**

**399. MHESHIMIWA LUCIA MICHAEL MLOWE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara:- Serikali imekuwa ikitoa ahadi juu ya

uanzishwaji wa mradi wa Mchuchuma na Liganga na Wananchi wana shauku sana na mradi huu:-

Je, ni lini sasa mradi huu utaanza.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:**

Kwamba, Bunge likubali kujadili Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2018 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kwamba, Bunge likubali kupitisha Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** — **S. KAGAIGAI**
**18 JUNI, 2019** — **KATIBU WA BUNGE**

PARLIAMENT OF TANZANIA
UHURU NA UMOJA
BUNGE LA TANZANIA